# Kijitabu cha Kanuni za Makaa Nchini Kenya

Kanuni zinazotumika sasa ili kudhibiti uzalishaji endelevu katika sekta ya makaa



## KANUNI ZA MAKAA

October 2012
Kimetayarishwa kwa niaba ya PISCES na Practical Action Consulting East Africa

Ingawa utafiti huu umefadhiliwa na idara ya Maendeleo ya Nchi za Kigeni (DFID) ya Uingereza, mitazamo iliyomo katika kijitabu hiki kwa jumla ni ya waandishi binafsi wala haiashirii msimamo au mitazamo ya DFID. Hivyo mijadala au maswali yote yaelekezwe kwa waandishi wala sio kwa DFID.

| | |
|---|---|
| **Waandishi wa nakala ya Kiingereza** | Tameezan wa Gathui<br>Frida Mugo<br>Wairimu Ngugi<br>Hannah Wanjiru<br>Sheila Kamau |
| **Mfasiri** | Omondi Dan Martin |
| **Wahariri** | Jamidu Katima (UDSM, Tanzania)<br>Rwaichi Minja (UDSM, Tanzania)<br>Agnes Mwakaje (UDSM, Tanzania)<br>Clement Ngoriareng (Huduma za Misitu nchini Kenya-KFS)<br>Francis Muchiri (Practical Action) |
| **Wachangiaji wa nakala ya Kiingereza** | Steven Hunt<br>Ewan Bloomfield (PAC, UK). |
| **Wahariri wa nakala ya Kiingereza** | Thomas Molony (Chuo Kikuu cha Edinburgh)<br>Katie Welford (PAC, UK)<br>Benard Muok (Taasisi ya Kufundishia Teknolojia ya Afrika (ACTS) |

**Picha kuu:** *Kitalu cha miti iliyopandwa na kikundi cha CSS, Bondo (Picha kwa hisani ya: Practical Action Consulting)*

**Picha ndogo:** *Makaa ya kuuza katika soko (Picha kwa hisani ya: Practical Action Consulting)*

**Picha zote:** *Zimepigwa na Practical Action ila ikielezwa vingine*

## Shukrani

Kijitabu hiki ni tafsiri kutoka nakala ya kiingereza iliandaliwa kupitia mchakato wa ushirika ukiongozwa na PAC kupitia mradi wa Mfumo wa Sera ya Ubunifu kwa ajili ya Usalama wa Nishati Safi (Policy Innovation Systems for Clean Energy Security-PISCES), mradi ambao ulifadhiliwa na DFID, Uingereza. PAC inashukuru mashirika ya kijamii (CBOs) ya Kitui na Bondo, wazalishaji wa makaa, wasafirishaji na wauzaji ambao walishiriki katika warsha ya PISCES mwaka wa 2009.

Vile vile tunawashukuru wadau wengine hasa Wizara ya Kawi; Wizara ya Misitu na Wanyama Pori kupitia KFS; Tume ya Kudhibiti Masuala ya Kawi (Energy Regulatory Commission); Taasisi ya Utafiti wa Misitu ya Kenya (KEFRI); Kikosi kazi ya Misitu cha Kenya (The Kenya Forest Working Group); CAMCO; Taasisi ya Kimataifa ya Ujenzi Vijijini (International Institute of Rural Reconstruction); ACTS; UDSM; ofisi ya Uingereza ya PAC; ofisi ya PAC eneo la Afrika Mashariki; na kikundi cha PAC kilichohusika katika kuandaa kijitabu hiki.

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| Mashirika ya Kijamii | Community Based Organizations (CBOS) |
| Chama cha Kijamii cha Misitu | Community Forest Association (CFA) |
| Kamati ya Kuhifadhi Misitu | Forest Conservation Committee (FCC) |
| Huduma za Misitu nchini Kenya | Kenya Forest Service (KFS) |
| Shilingi ya Kenya | Kenya Shilling (KES/Ksh) |
| Taasisi ya Utafiti wa Misitu ya Kenya | Kenya Forestry Research Institute (KEFRI) |
| Wizara ya Kawi | Ministry of Energy (MoE) |
| Wizara ya Misitu na Wanyama Pori | Ministry of Forestry and Wildlife (MoFW) |
| Shirika la Kutoa Ushauri la Practical Action Consulting | Practical Action Consulting (PAC) |
| Mfumo wa Sera ya Ubunifu kwa ajili ya Usalama wa Nishati Safi | Policy Innovation Systems for Clean Energy Energy Security (PISCES) |

## Misamiati

| | |
|---|---|
| Ufadhili | Kulipia au kugharamia |
| Muhtasari | Kwa ufupi |
| Wadau | Wahusika au washikadau |
| Mchakato | Mpangilio wa hatua kwa hatua wa kutekeleza jambo |
| Nishati | Kawi au nguvu kama ya upepo, umeme |
| Ufahamu | Kuelewa au kujulishwa jambo |
| Ada | Malipo, kiasi cha pesa kinachotozwa |
| Warsha | Mkutano wa kufundishia |
| Athari | Matokeo ya jambo au kitendo |
| Idhini | Ruhusa au kibali au ridhaa |

# Yaliyomo

**Shukrani** 2

**Vifupisho** 3

**Dhamira ya kijitabu cha kanuni za kudhibiti makaa** 5

**Sheria na Kanuni (Makaa) za Mwaka wa 2009** 7

Muhtasari wa Masharti na Wajibu: Wazalishaji/Wachomaji Makaa, Wasafirishaji, Wauzaji na Watumiaji

Chama cha Wazalishaji/Wachomaji makaa (Wadau)

Leseni ya Kuzalisha Makaa

Sheria za Usafirishaji wa Makaa

Sheria za Uuzaji wa Makaa

**Orodha ya ofisi za kanda za huduma za misitu nchini Kenya na maelezo ya mawasiliano** 17

**Fomu / zana zinazotumika na huduma za misitu nchini Kenya ili kuhakikisha kanuni za misitu (makaa) zinafuatwa** 21

i. Hati ya usajili wa chama

ii. Kutuma ombi la leseni ya kuzalisha/kuchoma makaa

iii. Idhini ya mmiliki wa shamba

iv. Kibali/hati ya kusafirisha makaa

v. Ombi la leseni/hati ya kuagiza na kuuza makaa nje

vi. Kibali/hati ya kuagiza / kuuza nje na viwango vya usafi



*Washiriki katika warsha ya kujifunza kusimamia miti katika shamba la Musaki, Kitengela*

# Dhamira ya Kijitabu cha Kanuni za Makaa

Madhumuni ya kijitabu hiki ni kuwarahisishia wadau katika sekta ya makaa nchini Kenya, hasa wazalishaji/wachomaji, wasafirishaji na wauzaji, kupatikana kwa mwongozo wa kisheria katika uzalishaji endelevu wa makaa. Kimeandaliwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali katika sekta ya makaa zikiwemo wizara na mashirika ya serikali, mashirika ya kiraia, mashirika ya kijamii pamoja na wafadhili miongoni mwa wengine. Kijitabu hiki ni tafsiri nyepesi ya Kitabu cha Sera za Makaa Nchini Kenya – Kanuni Zinazotumika Sasa ili Kudhibiti Uzalishaji Endelevu Katika Sekta ya Makaa (The Kenya Charcoal Policy Handbook – Current Regulations for a Sustainable Charcoal Sector), na ambayo hupatikana katika ofisi za Huduma za Misitu nchini Kenya (KFS) au kwenye tovuti ya PISCES (www.pisces.or.ke).

Makaa ni rasilimali muhimu sana na chanzo cha nishati nchini Kenya inayozalisha asilimia 82, na asilimia 34 ya kawi inayotumika katika jamii mijini na vijijini mtawalia kwa matumizi ya nyumbani.  Hutoa nafasi za ajira, na mapato kwa zaidi ya watu laki saba (700,000) ambao hutegemewa na zaidi ya watu milioni mbili. Ongezeko la watu, ukuaji haraka wa miji pamoja na maendeleo katika sekta ya ujenzi na samani zimeongeza maradufu mahitaji ya makaa.

Kati ya mwaka 2000 na 2009, Serikali ya Kenya kupitia Wizara ya Misitu na Wanyama Pori na Wizara ya Kawi, ilibuni sera na sheria za kudhibiti uzalishaji wa makaa (upandaji  wa miti na uchomaji wa makaa), usafirishaji, uuzaji na utumiaji. Matokeo yake, yalikuwa ni kutungwa kwa Sheria za Misitu Kifungu cha 7, ya mwaka wa 2005 sehemu ya 59 iliyopelekea kuundwa kwa kanuni za kudhibiti uzalishaji, usafirishaji na uuzaji wa makaa ambazo zilichapishwa katika gazeti rasmi la serikali kama Kanuni za Misitu (Makaa) za mwaka wa 2009. Utekelezwaji wa sera hiyo unaongozwa na Huduma za Misitu nchini Kenya chini ya Wizara ya Misitu na Wanyama Pori pamoja na Wizara ya Kawi zikishirikiana na mashirika ya serikali na wadau mbalimbali. Idara ya Huduma za Misitu ilibuni mikakati ya kuhakikisha sheria hizo zinafuatwa.Nakala za sheria hizo hupatikana bila malipo katika ofisi za Huduma za Misitu nchini Kenya katika kanda zote.

Mnamo mwaka wa 2009, shirika la PAC liliandaa warsha kama sehemu ya mradi wa PISCES ambayo ilihudhuriwa na wadau mbalimbali katika sekta ya makaa ambao walitambua umuhimu wa taarifa sahihi kuhusu sheria za makaa.

Warsha hiyo ilipendekeza:

- i. Kuwafahamisha watu kuhusu sera za makaa zinazotumika;
- ii. Kuundwa kwa Vyama thabiti vya wadau wa makaa;
- iii. Kuhimiza uwekezaji katika sekta hiyo ndogo;
- iv. Kupunguza kodi na idadi ya mamlaka za udhibiti wa sekta hiyo; na
- v. Kuondoa kodi haramu.

Kijitabu hiki kinashughulikia masuala kama:

- i. Kuongeza ufahamu wa watu kuhusu sera zinazotumika kama zilivyonakiliwa katika Sheria za Misitu (Makaa) za mwaka wa 2009;
- ii. Kuwaelimisha jinsi ya kuunda vyama vya wadau wa makaa; na
- iii. Kuwajulisha aina za kodi halali zinazofaa kulipwa kwa serikali na wazalishaji na wasafirishaji wa makaa kupitia idara ya Huduma za Misitu.

# Kanuni za Misitu (Makaa) za Mwaka wa 2009

## 1. Muhtasari wa Kutekeleza Kanuni pamoja na Wajibu: Uzalishaji, Usafirishaji, Uuzaji na Matumizi ya Makaa

| Masharti | Wajibu |
| --- | --- |
| **Uzalishaji** | |
| • Tathmini athari (za mradi wa makaa) kwa mazingira<br>• Zingatia upandaji wa miti na uhifadhi wa mazingira<br>• Kupanga mikakati ya usimamizi wa mapori ambamo miti huvunwa au kukatwa<br>• Hakikisha matumizi ya tanuru bora katika uzalishaji makaa | **Mzalishaji / anayechoma makaa**<br>• Apate idhini kutoka kwa mmiliki wa ardhi<br>• Apate mapendekezo ya kamati ya mazingira mashinani<br>• Atume ombi la leseni ya uchomaji makaa kwenye ofisi ya kanda ya Huduma za Misitu nchini Kenya<br>• Alipe ada maalum ya leseni[1]<br>**Afisa wa Huduma za Misitu nchini Kenya katika kanda**<br>• Kuthibitisha kufuatwa kwa masharti<br>• Kutoa hati / leseni ya uzalishaji makaa |
| **Usafirishaji** | |
| • Awe na hati ya asili ya makaa (makaa yalikotengenezwa)<br>• Awe na stakabadhi (risiti) za kuthibitisha amenunua kutoka kwa mzalishaji<br>• Awe na kibali cha usafirishaji makaa<br>• Awe na kibali cha kuagiza au kuuza makaa nje ya nchi kutoka kwa idara ya Huduma za Misitu | **Msafirishaji**<br>• Atume ombi la kibali cha usafirishaji makaa (zaidi ya magunia 3)<br>• Alipe ada ya leseni ya usafirishaji<br>**Afisa wa Huduma za Misitu nchini Kenya katika ukanda**<br>• Kuthibitisha kufuatwa kwa masharti yote<br>• Kutoa kibali cha kusafirisha makaa<br>**Polisi wa Trafiki**<br>• Kuthibitisha uhalali wa hati ya usafirishaji makaa<br>**Halmashauri ya Forodha (kuagiza na kuuza nje)**<br>• Kutoa hati/ kibali cha kuagiza au kuuza makaa nje ya nchi<br>• Kuthibitisha uhalali wa stakabadhi kwa mujibu wa kanuni za usalama wa makaa |
| **Uuzaji** | |
| • Nakala ya hati ya asili<br>• Nakala ya hati ya usafirishaji<br>• Leseni ya biashara au leseni ya serikali ya mitaa | **Muuzaji**<br>• Ahifadhi kumbukumbu za mahali alikotoa makaa (asili)<br>• Aweke nakala ya hati ya asili<br>• Aweke nakala ya hati ya usafiri<br>• Aoneshe / abandike leseni ya biashara / kibali toka kwa serikali ya mtaa au jimbo<br>**Afisa wa Kanda wa idara ya Huduma ya Misitu**<br>• Kukagua kumbukumbu/ stakabadhi za muuzaji |
| **Utumiaji** | |
| • Uhifadhi wa kawi | **Watumiaji**<br>• Kutumia jiko bora kama vile Kenya Ceramic Jiko<br>• Tumia mbinu za kitaalamu za kuhifadhi kawi kama kuloweka nafaka kavu kabla ya kupika, kutumia jiko lisilotumia moto, kufunika chungu au sufuria na kadhalika<br>• Watumiaji ni pamoja na jamii, familia, biashara ndogo ndogo, taasisi, na kadhalika |

[1] Tembelea ofisi za Huduma za Misitu katika kanda ilikupata taarifa kuhusu ada maalumu ya kila hati.

## 2. Chama cha Ushirika wa Wazalishaji / Wachomaji wa Makaa (Wadau)

Kanuni za Misitu (Makaa) za mwaka wa 2009 zinawataka wazalishaji/wachomaji makaa ya kuuza kuunda na kusajili Vyama vya Ushirika vya Wazalishaji Makaa (Charcoal Producers Associations - CPAs).

Majukumu ya Vyama vya Ushirika vya Wazalishaji/wachomaji Makaani pamoja na:

- Kuhimiza uzalishaji na uchomaji endelevu wamakaa.
- Kuhakikisha wanachama wote wanatekeleza mpango wa upandajiwa miti na kuhifadhi mazingira ili kuendeleza uzalishaji/ uchomaji makaa.
- Kujitungia miongozo sahihi ya uzalishaji/ uchomaji makaa ili kujidhibiti wao wenyewe.
- Kuisaidia idara ya Huduma za Misitu nchini Kenya katika kutekeleza masharti ya sheria za makaa kuhusu uchomaji endelevu wamakaa, usafirishaji na uuzaji.
- Kufanya kila jambo linalowezekana ili kuhimiza na kuendeleza uchomaji na usafirishaji wa makaa.



*Makaa yaliyoagizwa kutoka nchi jirani kupitia ziwa Victoria yakiuzwa kisiwani Ndunga, Kisumu*

### Hatua za kuunda chama cha ushirika wa wazalishaji/ wachomaji Makaa

i. Orodhesha wanachama wote na anwani zao;
ii. Tunga katiba na sheria zitakazofuatwa (wanaweza kutafuta usaidizi kutoka ofisi za kanda za Huduma za Misitu);
iii. Wajisajili kama chama kwenye ofisi ya msajili wa vyama vya ushirika.
iv. Oradhesha maeneo watakapofanyia shughuli zao;
v. Orodhesha kumbukumbu za kazi na shughuli za vikundi;
vi. Orodhesha maeneo watakaposafirisha makaa (kutoka wapi hadi wapi);
vii. Toa habari kuhusu umiliki wa shamba/ ardhi husika;
viii. Orodhesha shughuli zinazofanyika kwenye shamba/ardhi husika;
ix. Eleza aina ya teknolojia itakayotumiwa na kikundi kutengeneza makaa;
x. Eleza kiasi cha makaa kitakachozalishwa na kikundi;
xi. Eleza kikundi kina pesa ngapi kwa sasa, na ni kiasi gani kikundi kinategemea kutengeneza kutokana na makaa;
xii. Tuma ombi hilo kwa ofisi ya Huduma za Misitu ili kuratibiwa; na
xiii. Iwapo masharti yote yatafuatwa na taarifa zilizotolewa zitaridhisha, basi Huduma za Misitu itatoa hati ya usajili.



*Jiko linalotumia makaa*

## 3. Leseni ya Uzalishaji wa Makaa

i. Wakulima, wafanyabiashara, makampuni, mashirika na vyama vinavyozalisha / vinavyochoma makaa kwa minajili ya kuuza, sharti wapate kibali kutoka ofisi za Huduma za Misitu nchini Kenya kabla ya kuanza kuzalisha/kuchoma, kusafirisha au kuuza makaa.

ii. Chama cha kijamii kilichosajiliwa kinaweza kujihusisha na uzalishaji wa makaa. Hata hivyo, kitahitaji kuirekebisha katiba yake ili kuhakikisha inakidhi masharti yaliyotajwa hapo juu kuhusu vyama vya wazalishaji makaa.

iii. Wamiliki wa ardhi wanaozalisha makaa kwa matumizi yao ya nyumbani hawahitaji leseni.



*Vichaka vya miti ya Acacia vya Kikundi cha Kina Mama wa Masanga huko Rarieda, Nyanza*

### HATUA ZA KUPATA KIBALI CHA KUZALISHA/ KUCHOMA MAKAA

HATUA 1 Chukua fomu ya maombi kutoka ofisi ya kanda ya Huduma za Misitu nchini Kenyailiyo karibu au kutoka kwenye tovuti www.kenyaforestservice.org.

HATUA 2 Jaza fomu huku ukieleza habari zifuatazo:

- Mahali makaa yatakapozalishwa / yatakapochomwa.
- Mahali palipoidhinishwa ili kukusanya makaa.
- Aina ya miti itakayotumika kuzalisha/kuchoma makaa na idadi ya miti itakayotumika. Kumbuka kwamba hauruhusiwi kutumia miti ya asili au iliyo katika hatari ya kutoweka kwa mfano msandali (sandal tree).
- Mbinu za kiteknolojia zitakazotumika ili kuzalisha makaa kutoka kwenye miti, kwa mfano teknolojia ya kiasili au iliyoboreshwa – teknolojia iliyoboreshwa inapendekezwa kutumika ili kupunguza uharibifu wa miti, kwa sababu teknolojia iliyoboreshwa huzalisha makaa zaidi kutoka kwa idadi sawa ya miti kuliko mbinu za kiasili.

Aidha:

- Pata idhini ya mmiliki wa ardhi ambapo makaa yatazalishwa/ yatachomwa
- Pata mapendekezo kutoka kwa Kamati ya Shina ya Mazingira. Kamati hii sharti itathmini hali ya mazingira ili kuzuia kudunisha ardhi kama kupitia mmomonyoko wa udongo.
- Tengeneza mkakati wa kupanda miti na kuhifadhi mazingira; huu ni mpango unaoelezea ni jinsi gani miti itakayokatwa itarudishiwa kwa kupanda mingine



*Makaa hupakiwa katika vipimo tofauti*

HATUA 3 Tuma habari zilizonakiliwa awali (ii) kwa Kamati ya Kuhifadhi Misitu (FCC) na kulipa ada maalum. Ada hizi hubadilishwa kila baada ya muda fulani.

HATUA 4 Kamati ndogo inayoratibu maombi itatoa mapendekezo kwa Kamati ya Kuhifadhi Mazingira.

HATUA 5 Huduma za Misitu nchini Kenya itatoa kibali/leseni kulingana na mapendekezo ya Kamati ya Kuhifadhi Mazingira. Masharti ya leseni yanaweza kutofautiana kulingana na hali ya mazingira ya wakati huo.

**LESENI YA UZALISHAJI / UCHOMAJI MAKAA**

**Masharti ya leseni ya uzalishaji/ uchomaji**

- Usimpatie au kumhamishia mtu yeyote leseni yako ya uzalishaji.
- Kumbuka kulipia upya leseni yako ya uzalishaji ada maalum zinazotozwa kila mwaka au inavyoelekezwa kwenye leseni.
- Kumbuka kutuma ombi la kusajiliwa upya mwezi mmoja kabla ya muda wa leseni yako kumalizika.
- Usibadilishe au kumwandika mtu mwingine kinyume cha sheria ili atumie leseni yako.
- Usikubali kuzalisha makaa ya kuuza kwa kutumia leseni ya mtu mwingine.
- Usizalishe makaa kutumia miti ya asili au miti inayohifadhiwa kisheria.

**Idara ya Huduma za Misitu (KFS)**

- Itachapisha orodha ya miti iliyo hatarini kutoweka au inayohifadhiwa kisheria katika gazeti rasmi la serikali.
- Itasimamisha kwa muda au hata kutengua / kufutilia mbali leseni iwapo mwenyewe atakiuka masharti yaliyowekwa. Kumbuka:
  - i. Leseni ikisimamishwa kwa muda au kutenguliwa, mzalishaji sharti akome kuzalisha / kuchoma makaa hadi pale atakaporuhusiwa au kupewa leseni mpya.
  - ii. Iwapo mtu atanyimwa leseni kwa mujibu wa sheria, ni sharti aijiulishe kamati ndogo kila anapotuma ombi tena kwamba amewahi kunyimwa leseni awali.

**Jopo la Kitaifa la Mazingira**

Iwapo mtu, kampuni au chama hakijaridhishwa na uamuzi wa Huduma za Misitu kutokutoa leseni ya uzalishaji makaa, mhusika anaweza kukata rufaa kwa Jopo la Kitaifa la Mazingira (National Environment Tribunal).

## 4. Kanuni za Usafirishaji Makaa

Mahitaji ya kusafirisha makaa:

- Hati/ kibali / leseni halali ya kusafirisha makaa.
- Hati ya asili ya makaa kutoka kwa mzalishaji.
- Stakabadhi/risiti ya kuthibitisha umenunua kwa mzalishaji au muuzaji.

Wasafirishaji wa makaa wanahimizwa kujiunga na vyama vya ushirika vya wadau wa makaa ili wachangie uhifadhi wa mazingira, sera za serikali na mipango ya kitaifa ya upandaji wa miti.



**Adhabu:** Kusafirisha makaa bila kibali cha kusafirisha ni hatia yenye adhabu ya kutozwa faini isiyopungua shilingi elfu kumi (Ksh. 10,000) au kifungo cha miezi mitatu (3) gerezani. Hata hivyo Sheria ya Misitu ya mwaka wa 2005 ina adhabu kali zaidi kwa kosa hili; kutozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (Ksh. 50,000) au kufungwa gerezani miezi sita (6).

**HATUA YA KUPATA KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAKAA**

***Hatua 1: Msafirishaji***

| | |
|---|---|
| HATUA 1: Msafirishaji | Tembelea ofisi ya kanda ya Huduma za Misitu nchini Kenya na kupata fomu ya ombi inayohitaji taarifa zifuatazo:<br>• Kiasi cha makaa unayopanga kusafirisha.<br>• Sehemu asili ya kuchukulia makaa.<br>• Sehemu ambayo makaa yatapelekwa. Gari litakalotumika kusafirishia makaa; nambari ya usajili, aina ya gari nambari ya 'chassis'. |
| HATUA 2: Afisa wa Kanda wa idara ya Huduma za Misitu | Kukagua na kuthibitisha ombi. Iwapo ataridhishwa, atatoa kibali / hati ya usafirishaji makaa. Masharti ya hati hii ni:<br>• Huwezi kumpatia au kumhamishia mtu hati/kibali cha kusafirishia.<br>• Unaruhusiwa kusafirisha makaa kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni.<br>• Hakikisha umepata hati ya usafirishaji mapema ili muda wake usiishe kabla hujasafirisha makaa. |

## 5. Kanuni za Uuzaji wa Makaa

**SOKO LA NDANI**

- Muuzaji makaa kwa jumla au yule wa reja reja sharti:
  - i. Aweke kumbukumbu/rekodi ya sehemu makaa yalikochukuliwa.
  - ii. Aweke nakala ya hati ya sehemumakaa yalikochukuliwa.
  - iii. Aweke nakala ya hati ya usafirishaji.
- Hakuna mtu yeyote au chama chochote kitakacho fanya biashara ya makaana mzalishaji asiye na kibali.
- Afisa wa Huduma za Misitu nchini Kenya ana haki ya kutembelea mahali popote panapofanyiwa biashara ya makaa kwa jumla au rejareja ili kukagua stakabadhi.



**Adhabu:** Kununua au kuuza makaa kutoka kwa mataifa jirani kama vile Tanzania, Sudan, Uganda, na kadhalika, bila kibali ni hatia yenye faini isiyopungua shilingi elfu kumi (Ksh. 10,000) au kufungwa jela miezi mitatu.

**KUUZA MAKAA NJE YA KENYA**

- Mtu yeyote au chama chochote kitachotaka kuuza makaa nje ya Kenya, sharti awe na kibali cha kuagiza na kuuza nje kutoka idara ya Huduma za Misitu.
- Mtu yeyote anayenuia kupata hati ya kuagiza na kuuza makaa nje ya nchi sharti atume ombi kwa Mkurugenzi, Huduma za Misitu nchini Kenya huku akieleza kinaganaga sehemu atakayochukulia makaa/chanzo cha makaa yake (asili).
- Kwa kuidhinisha ombi, mkurugenzi atatoa kibali cha kuagiza au kuuza nje ya nchi, hati ya usalama baada ya mwenye ombi kulipa ada husika.
- Leseni ya kuuza nje au kuagiza na hati ya usalama:
  - i. Zitapewa afisa wa forodha kwenye mpaka wa kuingizia au kutoa makaa au pale mfanyibiashara atakapohitaji hati ya kuagiza pamoja na hati ya usalama;
  - ii. Hati ya kuagiza au kuuza nje pamoja na hati ya usalama zote

zitapigwa muhuri kwenye mpaka ;

iii. Muda wa stakabadhi hizi mbili (hati ya kuagiza na kuuza nje na hati ya usalama) huisha punde tu makaa inapopakiwa kwenye chombo cha kusafirishia makaa au tarehe iliyoandikwa kwenye stakabadhi; kimojawapo kitakachotangulia.

## KUAGIZA MAKAA KUINGIA KENYA

- Hakuna mtu au chama kitakachoagiza makaa au bidhaa za makaa kuja Kenya bila kibali kutoka Huduma za Misitu.
- Yeyote anayenuia kuagiza makaa sharti atume ombi la kupewa hati ya kuagiza huku akitoa maelezo ya chanzo cha makaa yake kwa kamati husika.
- Kamati husika ya Huduma za Misitu baada ya kulijadili ombi hilo, itatuma pamoja na mapendekezo yao kwa Mkurugenzi wa Huduma za Misitu nchini Kenya, huku wakizingatia hali ya mahitaji na kupatikana kwa makaa nchini.
- Mkurugenzi akiliidhinisha ombi hilo, basi atatoa hati ya kuagiza baada ya mwenye ombi kulipa ada husika.

## UKAGUZI WA HUDUMA ZA MISITU (KFS)

- Afisa wa misitu anaruhusiwa kukagua maeneo na vifaa vya uzalishaji / uchomaji makaa, usafirishaji, na biashara / uuzaji:
  i. Mara kwa mara;
  ii. Anaposhuku masharti hayajafuatwa / yanakiukwa;
  iii. Inapofaa ili kutoa leseni ya kuagiza.
- Anayepewa kibali/leseni ataipeana/ataitoa leseni kwa kufuata masharti yaliyotajwa kwa afisa wa Huduma za Misitu nchini Kenya atakapoitishwa.
- Ikiwezekana, afisa wa Huduma za Misitu atafanya ukaguzi wa kushtukiza bila kutoa taarifa.
- Huduma za Misitu nchini Kenya inaweza kufuta leseni au hati ya mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa mujibu wa kanuni hizi.
- Bila idhini ya bodi ya Huduma za Misitu nchini Kenya, yeyote atakayepatikana na hatia kwa mujibu wa sheria hizi hatapewa leseni au hati chini ya masharti ambayo ameyakiuka kwa muda wa mwaka moja tangu kupatikana na hatia.
- Mtu yeyote atakayepatikana na hatia na leseni au hati yake kufutiliwa mbali atahitajika kuisalimisha leseni au hati hiyo katika ofisi ya Huduma za Misitu nchini Kenya kabla ya siku kumi na nne (14) kupita.

# Orodha ya Ofisi za Kanda za Huduma za Misitu nchini Kenya, na Maelezo ya Mawasiliano

| Eneo la Misitu / Kanda | Meneja wa Kanda[2] – Huduma za Misitu nchini Kenya | Saduku la Posta (S. L. P.) | Simu ya Mkononi (Nambari) |
|---|---|---|---|
| Baringo | TOO, Daniel Kiplimo | S. L. P. 54 Kabarnet | 0729-811144 |
| Bomet | MBURU, James Mwangi | S. L. P. 304 Bomet | 0722-888489 |
| Bondo | OMARE, James Momanyi | S. L. P. 451 Bondo | 0729-030201 |
| Bungoma | CHANGAMU, Thomas Osea | S. L. P. 506 Bungoma | 0710-955633 |
| Buret | RONO, John Kipkemoi | S. L. P. 783 Litein | 0722-117482 |
| Busia | WERE, James Osewo | S. L. P. 111 Busia | 0726-173761 |
| Embu | WAWERU, Samuel Nderitu | S. L. P. 2 Embu | 0727-884724 |
| Garissa | HUSSEIN, Noor Maalim | S. L. P. 89 Garissa | 254-462352 |
| Gucha | UNWA, Jorame Kioko | S. L. P. 122 Ogembo | 0720-485532 |
| Homa Bay | KIOKO, Peter Mutua | S. L. P. 46 Homa Bay | 0710-373577 |
| Ijara | AMBIA, Abdi Osman | S. L. P. 5 Masalani | 0720-969074 |
| Isiolo | NZOU, Jackson Kiluli | S. L. P. 141 Isiolo | 0728-737474 |
| Kajiado | KURGAT, Alfred Kipchumba | S. L. P. 229,Kajiado | 0722-241911 |
| Kakamega | MURAGURI, Mwai | S. L. P. 1233, Kakamega | 0722-676627 |
| Keiyo | KERENGO, Dennis Kiprotich | S. L. P. 397 Iten | 0722-341440 |
| Kericho | MANYALA, Caleb Kaduki | S. L. P. 1 Londiani | 0722-865373 |
| Kiambu | NJENGA, George Ndung'u | S. L. P. 74 Kikuyu | 0723-629348 |
| Kilifi | MAINA, Christopher Muema | S. L. P. 247 Kilifi | 0721-412255 |
| Kirinyaga | MISONGE, Francis Mariera | S. L. P. 22 Kerugoya | 0722-228623 |
| Kisii Central | MWANZIA, David Kavyu | S. L. P. 775 Kisii | 0722-876328 |
| Kisumu | KIBUKA, Erastus Ngunguru | S. L. P. 1048 Kisumu | 0711-310217 |
| Kitui | WANYIRI, Maurice Wanjohi | S. L. P. 106 Kitui | 0734-901386 |
| Koibatek | MUSYOKA, Anthony Kioko | S. L. P. 28 Eldama Ravine | 0722-224893 |
| Kuria | MUKHWANA, James Shikuku | S. L. P. 269 Kihancha | 0722-104272 |
| Kwale | IMBWAGA, Gilbert Mugei | S. L. P. 5 Kwale | 0720-226267 |
| Laikipia | CHEPTOO, William Kiprotich | S. L. P. 8 Nyahururu | 0710-475460 |
| Lamu | MAINA, Joseph Matu | S. L. P. 49 Lamu | 0721-222343 |
| Lugari | MWANGI, Stanley Irungu | S. L. P. 42 Turbo | 0725-872690 |
| Machakos | WAMALWA, Jenipher Nasombi | S. L. P. 2 Machakos | 0726-607864 |
| Makueni | RUKUNGU, James Chomba | S. L. P. 395 Makueni | 0721-436783 |
| Malindi | ORINDA, Bernard Okech | S. L. P. 201 Malindi | 0722-933802 |
| Mandera | MOHAMED, Adan Mohamed | S. L. P. 65 Mandera | 0720-805684 |
| Marsabit | KAINDI, Francis Mutiso | S. L. P. 27 Marsabit | 0727-855685 |
| Mbeere | MUTHEMBWA, James Mutuvi | S. L. P. 220 Siakago | 0724-844820 |
| Meru Central | MANENO, Evans | S. L. P. 281 Nakuru | 0722-473467 |
| Meru North | KAHUNYO, Stephen Wambugu | S. L. P. 390 Maua | 0722-432098 |
| Meru South | WAKIAGA, Joseph | S. L. P. 210 Chuka | 0722-489603 |
| Migori | MBOGA, Timon Otieno | S. L. P. 30513-00100,Nbi | 0722-738292 |
| Mombasa | WAMOLA, Charles Mwadime | S. L. P. 80078 Mombasa | 0726-345898 |
| Moyale | CHEMITEI, Erick Kiplagat | S. L. P. 37 Moyale | 0722-785532 |
| Mt Elgon | OMBIRI, Wilson Okanda | S. L. P. 88 Kapsokwony | 0722-553896 |
| Mumias | AVUDE, Donald Chunguli | S. L. P. 265 Butere | 0711-600252 |
| Muranga North | GITONGA, James Muchemi | S. L. P. 8 Nyahururu | 0722-331025 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Murang'a South | OWATE, Augustine Omamo | S. L. P. 76 Kigumo | 0722-595886 |
| Mwingi | MUTETO, Elijah Muasya | S. L. P. 5 Msalani | 0736-833277 |
| Nairobi | NJOROGE, John | S. L. P. 30513-00100 Nairobi | 0722-345473 |
| Nakuru | MUKUNDI, Samuel Kimani | S. L. P. 25 Elburgon | 0722-647999 |
| Nandi North | SERONEY, Rosemary Jebet | S. L. P. 235 Kapsabet | 0722-962226 |
| Nandi South | NYABUTI, Albert Omondi | S. L. P. 132 Nandi Hills | 0722-953454 |
| Narok | CHARANA, Joshua Nyarondia | S. L. P. 34 Narok | 0722-567391 |
| North Rift Conservancy | NYASWABU, Alfred Nyairo | S. L. P. 41 Eldoret | 0721-558963 |
| Nyamira | AMINO, Dennis Josiah | S. L. P. 46 Nyamira | 0711-600699 |
| Nyandarua | KINYILI, Benjamin Mutuku | P.O Box 289 Ol'kalau | 0723-393737 |
| Nyando | MWAURA, Geoffrey Karanja | S. L. P. 125 Ahero | 0723-405841 |
| Nyeri | MATHINJI, Francis Muchiri | S. L. P. 28 Nyeri | 0733-809950 |
| Rachuonyo | MCOOKO, George Sijenyi | S. L. P. 534 Oyugis | 0722-880503 |
| Siaya | SOI, Andrew Cheruiyot | S. L. P. 376 Siaya | 0727-405277 |
| Suba | MBAABU, Jonah | S. L. P. 107 Mbita | 0722-340506 |
| Taita Taveta | ONGERE, Allan Ojwang' | S. L. P. 1043 Wundanyi | 0721-495029 |
| Tana River | ABUTO, George Omolo | S. L. P. 18 Hola | 0722-976248 |
| Teso | KITUM, Elijah Murkomen | S. L. P. 29 Amagoro | 0722-880073 |
| Tharaka | GONDO, Anthony Mwangi | S. L. P. 210 Chuka | 0733-854561 |
| Thika | KINYANJUI, Anthony Kimani | S. L. P. 1197 Thika | 0721-723989 |
| Trans Mara | MASIBO, Monica Mbatha | S. L. P. 114 Kilgoris | 0722-263580 |
| Trans Nzoia | WAHOME, Simon Kimani | S. L. P. 99 Kitale | 0721-986452 |
| Turkana | KILIMO, Enoch Yano | S. L. P. 39 Lodwar | 0735-518009 |
| Uasin Gishu | KARANJA, Paul Ndungu | S. L. P. 41 Eldoret | 0722-265029 |
| Vihiga | OGUTU, Mathews Ooko | S. L. P. 781 Maragoli | 0722-336596 |
| West Pokot | KARIUKI, Gabriel Macharia | S. L. P. 42 Kapenguria | 0733-232117 |

[2] Viongozi wa Huduma za Misitu ya Kenya katika kanda waweza kuhamishwa katika maeneo mbali mbali mara kwa mara

# Sampuli za Fomu/Zana Zinazotumika na Huduma za Misitu nchini Kenya ili Kuhakikisha Kanuni za Misitu (Makaa) Zinafuatwa

## Hati Ya Usajili Wa Chama

**FOMU 1** **(r.5(2))**

Nambari ya kumbukumbu……………………………..

SHERIA ZA MISITU, 2005

HATI YA USAJILI WA CHAMA

1. Jina la chama……………………………………………………………………
2. Nambari ya kodi (PIN)…………………………
3. Idadi ya wanachama………………………………………………………………
4. Anwani kamili………………………………………………………………...……
5. Eneo la chama…………………………………………………………….
6. Sehemu ya Uhifadhi………………………....Wilaya…………………………
7. Kata……………………………………….….. Kijiji…………………………

Kimesajiliwa kama chama cha ushurika cha wazalishaji wa makaa kwa minajili ya uzalishaji/uchomaji makaa endelevu kwa mujibu wa masharti ya Sheria za Misitu (makaa) ya mwaka wa 2005 na kanuni za sheria hiyo na kutilia maanani masharti yafuatayo:………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

Ada zilizolipwa (kwa maneno)…………………………… kwa tarakimu…………......................................................................

Tarehe ya kutolewa………………….

Hadi tarehe 31 Desemba…………………

……………………………………………………..

Mkurugenzi, Huduma za Misitu

SAMPULI

## Ombi La Kupewa Leseni Ya Uzalishaji / Uchomaji Makaa

**FOMU 2** **(r.7(2))**

Nambari ya kumbukumbu……………

**OMBI LA LESENI YA KUZALISHA / KUCHOMA MAKAA**

**SEHEMU YA HABARI ZA MWENYE OMBI**

A1. Jina la mwombaji / mwenye kupewa leseni (chama au biashara)………………………
Nambari ya hati ya usajili…………………………
A2. Nambari ya kodi (PIN)……………………………………………
A3. Anwani kamili……………………………………………………...

**SEHEMU YA B: HABARI ZA LESENI INAYOTUMIKA**

B1. Jina la mwenye leseni inayotumika sasa………………………………………….
………………………………………………………………………………………
B2. Eneo na tarehe ya kutolewa kwa leseni ya
makaa inayotumika……………………….……………………………………………………

**SEHEMU YA C. MASHARTI YA KUZINGATIWA**

C1. Eneo au maeneo makaa yatakapozalishwa /
yatakapochomwa makaa……………………………………………………………………………………
C2. Mahala teule pa kukusanyia makaa………………………………………………………………….
C3. Idhini ya mmiliki wa ardhi/ shamba, ilivyoainishwa katika
fomu3 ……………………………………………………………………………………………
C4. Aina ya miti itakayotumika kuzalisha/kuchoma makaa……………………..
…………………………………………………………………………………………….
C5. Aina ya teknolojia/utaalamu utakaotumika……………………..……………
C6.Mapendekezo kutoka kamati shina ya mazingira …………………………
…………………………………………………………………………………………….
C7. Mipango ya upandaji wa miti na uhifadhi wa
Eneo……………………… Jina………………………………………… Cheo……………………………………………
Sahihi………………………………………………………………………………….
Kwa niaba ya …………………………………………………
Jina na muhuri wa chama/kampuni………………………………. Tarehe……../.....

**SEHEMU YA D. TAMKO LA ANAYEOMBA LESENI**

Ninathibitisha kwamba maelezo yaliyotolewa hapa ni ya kweli na hakika ninavyojua na kuamini. Ninaelewa kwamba leseni ya makaa inaweza kusimamishwa kwa muda, kubadilishwa, kutenguliwa au kufutiliwa mbali iwapo taarifa nilizotoa zitagunduliwa kuwa sio za kweli, zinapotosha, za uongo au si kamililifu.

**SEHEMU YA E: KWA MATUMIZI YA OFISI**

Imeidhinishwa/Haijaidhinishwa………………………………………………………
Maelezo………………………………………………………………………………………
Afisa………………………… Sahihi………………………… Tarehe…………..
Ada (kwa maneno)……………………..kwa tarakimu…………………………
Tarehe ya kutolewa……………………

.........................................................................
Mkurugenzi, Huduma za Misitu

SAMPULI

## Idhini Ya Mmiliki Wa Ardhi / Shamba

### FOMU 3 (r.7(4))

**SHERIA ZA MISITU, 2005**

**SEHEMU A: MWENYE KUOMBA IDHINI**

A.1 Jina la mwenye kuomba Idhini (chama au kampuni)………………..

Nambari ya usajili…………………………………………………….

A.2 Nambari ya kodi (PIN) ……………………………………………………

A.3 Anwani kamili ………………………………………………………………

**SEHEMU YA B: MWENYE KUTOA IDHINI**

B.1 Jina la mmiliki ardhi au mwakilishi wake……………………………

B.2 Nambari ya binafsi ya kitambulisho (PIN)…………………………..

B.3 Anwani kamili …………………………………………………………….

**SEHEMU YA C: TANKO LA MMILIKI ARDHI/ MWAKILISHI WAKE**

Nimeidhinisha Chama au Kampuni iliyotajwa hapo juu kuzalisha makaa katika ardhi yangu kwa kutumia rasilimali asili au miti iliyopandwa kulingana na vipengele vya Sheria ya Misitu, 2005, Kanuniza Misitu (Makaa) pamoja na vigezo vifuatavyo:……..
..................................................................………………

………………………………………………………………………………………

Jina…………………………… Mmiliki shamba………………..……..Sahihi………………..

Kwa niaba ya ……………..Muhuri wa chama/ kampuni………….Tarehe……

**SEHEMU D: MATUMIZI YA OFISI**

Imeidhinishwa/ Haijaidhinishwa…………………………………………………

Maelezo ……………………………………………………………………………..

Afisa ………………………………………….Sahihi ……………….. Tarehe……..

…………………………………….

Mkurugenzi, Huduma za Misitu

SAMPULI

## Kibali Cha Kusafirisha Makaa

## FOMU 4 (r.14(3)

### KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAKAA

Hifadhi ………………………………… Wilaya…………………………………

Kata/ Taarafa………………………………………………………………….

Jina …………………………………Anwani …………………………………

Uraia ………………………………. Nambari yakitambulisho / pasi………..

Ameruhusiwa kusafirisha makaa na bidhaa zake kama ifuatavyo:

Makaa/ Bidhaa Zake Kiasi

Kutoka Kwenda/ hadi

Hifadhi Mahali/ eneo Hifadhi Eneo

Sababu za kusafirisha ……………………………………………………………

Tarehe ya kusafirisha ………………………………Hadi tarehe………………

Nambari ya risiti/ stakabadhi ya malipo……………………………………………

Jina la afisa wa Huduma za Misitu aliyetoa ………………………………………

Cheo……………………………Sahihi………………………Tarehe ………..

Jina la afisa wa misitu anayesimamia ………………………………………………...

Cheo……………………........................................................................................

Sahihi …………………………………… Tarehe ………………………………….

Ada kwa maneno ………………………. Kwa tarakimu………………………….

Tarehe ya kutolewa ……………………

……………………………………………

Mkurugenzi, Huduma za Misitu

SAMPULI

## Ombi La Hati/kibali Cha Kuagiza Au Kuuza Nje

## FOMU 5 (r.16, 17)

**SHERIA YA MISITU, 2005**
**OMBI LA KIBALI/HATI KUAGIZA MAKAA AU KUUZA NJE**

**SEHEMU A: HABARI ZA MWENYE OMBI**
A1. Jina la mwenye kuomba (chama/kampuni)……………………………………
A2.Nambari ya usajili…………………………………………………………………
A3. Nambari ya kodi (PIN)………………………............................................
A4. Anwani kamili…………………………………………………………………….
A5. Eneo la biashara (nyumba /eneo)……………………………………………..
Nambari ya hati miliki……………………….Mtaa /barabara…………………….
Mji ……………………………………………………Wilaya……………………………..

**SEHEMU B: TAARIFAZA BIASHARA**
B1. Tofauti na biashara hii ambayo unaiombea kibali, je unafanya biashara yoyote katika sekta ya misitu?
Ndiyo/Hapana ……………………………………………………………………
B2. Iwapo jibu la B1 ni ndiyo, tafadhali eleza aina ya biashara………………
……………………………………………………………………………………………….

Makaa na bidhaa zake Kiasi Thamani

B4. Jina na Anwani ya mwenye kutuma/kupokea ………………………………..
…………………………………………………………………………………………………….

**SEHEMU C: MASHARTI YA USAFI**
C1. Je makaa unaotaka kuagiza/kuuza nje umekidhi/umefikia kiwango cha usafi? Ndiyo/Hapana ………………………………………………………
C2. Je makaa hauna moto na ni salama kusafirisha?
Ndiyo……………………………….. /Hapana ……………………………
C3. Ikiwa jibu la C1 na C2 ni ndiyo, Eleza hatua/mikakati ya kuhakikisha makaa hauna moto wala hatari yoyote……………………………………………

**SEHEMU D: TAMKO LA MWENYE OMBI**
Mimi/Sisi ninaapa / tunaapa kwamba taarifa tulizotoa hapa ni za kweli, hakika. Ninaelewa / tunaelewa wazi wazi kugunduliwa kwa taarifa za uongo kutatufanya kunyimwa leseni.

Sahihi……………………………………Tarehe……………………………………
Jina la mwenye sahihi……………………………………………………………………
Cheo katika (chama/kampuni)……………………………………………………….

**SEHEMU E: MATUMIZI YA OFISI**
Imeidhinishwa/Haijaidhinishwa…………………………………………………
Maelezo…………………………………………………………………………………
Afisa……………………………Sahihi……………………Tarehe………………….
Ada (kwa maneno)……………………………… kwa tarakimu…………………
Tarehe ya kutolewa……………………………………………………………………..
Mkurugenzi, Huduma za Misitu

SAMPULI

## Kibali Cha Kuagiza Makaa/kuuza Nje Kwa Kufuata Masharti Ya Usafi

**FOMU 6** (r.16, 17)

**KIBALI CHA KUAGIZA MAKAA / KUUZA NJE KWA KUFUATA MASHARTI YA USAFI**

Kwa: Afisa wa Forodha

Halmashauri ya Ukusanyaji Ushuru……………………………………………………..

(Sehemu ya Mpaka / Bandari / Uwanja wa ndege - kusafirisha makaa nje)

Hii ni kuthibitisha kwamba (jina)………………………………………………………….wa(anwani)………………………… ………………………………….ameidhinishwa kuagiza/kuuza makaa nje makaa/bidhaa za makaa uliotajwa hapa chini kutoka………………………………../ hadi (nchi)……………………………………..

| Makaa / bidhaa zake | Kiasi | Thamani |
|---|---|---|
| | | |
| | | |

Jina na amwani ya mwenye kutuma………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………….

SAMPULI

Kwa zaidi ya miaka arubaini, PAC imekuwa ikitoa ushauri wa kitaaluma kuhusu maendeleo ikiwa ndilo tawi la "International Non-governmental Organization" la mashauriano, "Practical Action" awali ikiitwa "Intermediate Technology Development Group." PAC hutoa ushauri wa kitaaluma ya hali ya juu kwa serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya kutoa misaada pamoja na sekta ya kibinafsi. Tunafanya kazi kote ulimwenguni tokea ofisi zetu za Uingereza, Mashariki na Kusini ya Afrika, Kusini ya Asia na Merikani ya Kilatini. Maono yetu ni ya ulimwengu endelevu pasi na umaskini na udhalimu ambamo teknolojia hutumika kuwafaidi wote. Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti www.practicalaction.org/consulting.

ACTS inatambulika kama kikundi cha kwanza cha kiafrika cha wataalamu ambao walielekeza taaluma ya sayansi na teknolojia katika maendeleo. Waanzilishi wa ACTS walikuwa na maono ya shirika ambalo lingeelekeza Afrika kutoka kwenye lindi la umaskini na uhuru kuelekea magharibi kwenye maendeleo ya kina, nia yao kuu ikiwa maendeleo huku ikishawishi uundaji wa sera zitakazoweka Afrika kwenye ramani mbalimbali, zinazojadili teknolojia mpya zinazochipuka na maswala ya nishati asili, usafi wa kiasili, mabadiliko ya hali ya hewa na mazingira. Kwa maelezo zaidi tembelea http://www.acts.or.ke

Ikiongoza utafiti wa misitu, KEFRI ni taasisi ya umma iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria za Sayansi na Teknolojia chini ya Sura 250 ya katiba ya Kenya. Wajibu wa KEFRI ni kufanya utafiti wa misitu, kushirikiana na mashirika mengine ya utafiti nchini na kimataifa ambayo yanafanya utafiti sawia na KEFRI, kuwasiliana na mashirika na taasisi za elimu ya kuwafundisha watu juu ya tafiti za misitu na pia kusambaza habari au matokeo ya tafiti hizo. Wajibu wake ni kuimarisha hali ya jamii na kuichumi ya Wakenya kwa kutumia utafiti kuendeleza na kukuza misitu na rasilimali nyinginezo. Kwa maelezo zaidi tembelea http://www.kefri.org

KFS ni taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria za Misitu, 2005, yenye jukumu la kuchangia maendeleo ya sekta ya nishati na rasilimali kwa kuhimiza maendeleo, uhifadhi, na usimamizi wa rasilimali za misitu ya Kenya. KFS ina idara tano za kitaifa zinazohusika katika utekelezaji: usimamizi na uhifadhi wa misitu ya kiasili, upandaji wa misitu, shughuli za kibiashara na utoaji wa vibali; mtandao wa misitu; utekelezwaji wa sheria; mashirika. Majukumu mengine ya Huduma za Misitu ni pamoja na kuhimiza usimamizi na uhifadhi wa misitu kupitia Vyama vya Kijamii vya Misitu (CFA) kutoa vibali vya kutekeleza shughuli mbalimbali na usimamizi wa uhifadhi kupitia hifadhi kumi za maeneo zikiwa na kamati moja ya kuhifadhi misitu (FCC) kila moja. Kwa taarifa zaidi http://www.kenyaforestservice.org.

PISCES ni mradi wa utafiti wa miaka mitano unaofadhiliwa na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza. Utekelezwaji wake ulianza Julai 2007. Dhamira ya mradi huu ni kuongoza maarifa na ufahamu wa sera zinazohusiana na ubadilishanaji au matumizi kwa awamu ya nishati, chakula, maji, kukimu maisha zikilinganishwa na nishati ya kiasili au ya kibaiolojia. PISCES ni utafiti unaounganisha Kituo cha Kusomea Teknolojia ya Afrika (ACTS, Kiongozi wa Utafiti), Kenya; shirika la Practical Action Consulting Uingereza - Mashariki ya Afrika na Sri Lanka; Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Tanzania; Wakfu wa Utafiti wa M.S Swaminathan (MSSRF), India; na Chuo Kikuu cha Edinburgh Uingereza. www.pisces.or.ke